



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Email- [ded.itigidc@singida.go.tz](mailto:ded.itigidc@singida.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi  
01 Barabara ya Halmashauri  
S.L.P 70,  
43483 ITIGI - SINGIDA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HW/ITG/S1/22 VOL IV/27

27 Novemba, 2023.

Kwa wananchi wote

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023 yenye Kumb.Na. FA.97/228/01'TEMP/06 cha tarehe 06 Aprili, 2023 Kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi iliyotangazwa hapo chini.

#### 1. MWANDISHI MWENDESHA OFISI (KATIBU MAHSUSI) DARAJA LA II – (NAFASI 3)

##### Kazi na Majukumu ya Katibu Mahsusni

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na Siri
- Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- Kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine.
- Kutafuta Majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo sehemu husika.
- Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya Vikao mbalimbali; na
- Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi.

## Sifa za Mwombaji

- Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA Level 6 ya uhazili.
- Awe amehudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu
- Awe amefaulu Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Excel, Powerpoint, Internet, E – mail na Publisher.

## Mshahara

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS C kwa Mwezi

### 1. MASHARTI KWA UJUMLA

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45)
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe na maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha (IV na VI), na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- **“Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA**
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **11 Disemba, 2023 saa 9:30 Alasiri**

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi  
01 Barabara ya Halmashauri  
S.L.P 70,  
43483 ITIGI - SINGIDA.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



John K. Mgalula

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**

**Nakala:** Katibu,

Ofisi ya Rais,

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,

S.L.P 2320,

**DODOMA.**

- Mbao za Matangazo